THE UNIVERSITY OF KANSAS HEALTH SYSTEM

# Taarifa ya Mbinu za Faragha

Taarifa hii inaeleza jinsi maelezo yako ya matibabu yanavyoweza kutumika na kufichuliwa na jinsi unavyoweza kufikia maelezo haya.

TAFADHALI ISOME KWA MAKINI!

*Tarehe ya kuanza kutumika: Tarehe 14 Aprili 2003*
*Tarehe ya kusahihishwa: Desemba 21, 2025*

**TAARIFA HII YA MBINU ZA FARAGHA INAHUSU MASHIRIKA YAFUATAYO:**

Taarifa hii inaeleza mbinu za faragha za watoa huduma za afya waliotajwa hapa chini wanaoshiriki katika mfumo wa The University of Kansas Health System Organized Health Care Arrangement (OHCA). OHCA ni mfumo wa kimatibabu uliojumuishwa ambapo watu hupokea huduma za afya kutoka kwa zaidi ya mtoa huduma mmoja au mfumo uliopangwa wa huduma za afya ambapo kuna zaidi ya mtoa huduma mmoja wa afya anayeshiriki.

The University of Kansas Health System Organized Health Care Arrangement inafafanuliwa kama:

- The University of Kansas Health System ikijumuisha:
    - University of Kansas Hospital Authority na washirika
    - UKHS Great Bend, LLC na washirika
    - Olathe Medical Center, Inc. na washirika
    - Miami County Medical Center, Inc. na washirika
    - New Liberty Hospital Corporation na washirika
    - Wafanyakazi na watoa huduma za afya waliopewa vyeti na wafanyakazi wa huduma za afya
- The University of Kansas Physicians
- The University of Kansas Medical Center

Watoa huduma hawa wanajumuisha, wafanyakazi, wakandarasi, wakurufunzi, makundi ya wanaojitolea, wanafunzi na watoa huduma wengine wa afya, wakiwemo wafanyakazi wa huduma ya matibabu wanapotoa huduma ya matibabu katika vituo vya mfumo wa huduma za afya. Washiriki, vituo na maeneo haya yote yanafuata masharti ya Taarifa hii. Zaidi ya hayo, huluki, vituo na maeneo haya yanaweza kutumiana maelezo yako ya afya kwa ajili ya matibabu, malipo na/au shughuli za huduma ya afya kama inavyoelezwa katika Taarifa hii.

Kwa pamoja, washiriki hawa watarejelewa kama “sisi” au “nasi” katika Taarifa hii. Tunaweza kutumiana maelezo ya matibabu kwa ajili ya matibabu, malipo au kwa madhumuni ya uendeshaji wa shughuli. Sheria inaturuhusu tufanye hivyo ili kutoa huduma bora za afya. Isitoshe, watoa huduma za afya wengine katika mfumo wa The University of Kansas Health System Organized Health Care Arrangement wanaweza

kushiriki katika mitandao ya matibabu iliyojumuishwa kwa makusudi ya ukaguzi wa matumizi ya pamoja, utathmini wa ubora na uboreshaji, au shughuli za malipo, na watoa huduma hao wanaweza kutumiana maelezo hayo ya afya na washiriki wa mtandao kama inavyohitajika ili kutekeleza shughuli za pamoja za mtandao.

## Kanusho Muhimu

Watoa huduma waliotajwa hapo juu wanakupa Taarifa hii ya pamoja. Kila mtoa huduma aliyetajwa katika Taarifa hii ya pamoja ni mtoa huduma za afya binafsi. Kila mtoa huduma anawajibika kibinafsi kwa shughuli zake binafsi. Hii inajumuisha kutii sheria za faragha na huduma zote za afya anazotoa. Hatutoi huduma za afya kwa pamoja au kwa niaba ya kila mmoja. Tunaweza kutuma maelezo ya afya kama inavyoruhusiwa na sheria.

**HAKI ZAKO**

*Una haki ya:*

- Kupata nakala ya karatasi au ya kielektroniki ya rekodi yako ya matibabu
- Kuomba kurekebishwa kwa rekodi yako ya matibabu ya karatasi au ya kielektroniki
- Kuomba mawasiliano mbadala
- Kutuomba tupunguze maelezo tunayotuma
- Kupata orodha ya washiriki tuliowatumia maelezo yako
- Kupata nakala ya Taarifa hii ya faragha
- Kuchagua mtu wa kuhusishwa katika huduma yako ya matibabu
- Kuwasilisha malalamiko ikiwa unaamini kuwa haki zako za faragha zimekiukwa

**CHAGUO ZAKO**

*Unaweza kuchagua jinsi tunavyotumia na kutuma maelezo yako tunapo:*

- Waambia wanafamilia au marafiki kuhusu hali yako
- Toa msaada wa janga
- Kujumuisha kwenye saraka ya hospitali
- Toa huduma za tiba ya kisaikolojia
- Tangaza huduma zetu
- Changisha pesa
- Uza maelezo yako – Inahitaji idhini yako

**UFICHUZI NA MATUMIZI YETU**

*Tunaweza kutumia na kutuma maelezo yako tunapo:*

- Kukutibu
- Endesha shirika letu
- Tuma bili za huduma
- Saidia katika masuala ya afya na usalama wa umma
- Fanya utafiti
- Tii sheria
- Jibu maombi ya kuchanga viungo na tishu
- Shirikiana na mchunguzi wa kimatibabu au mwelekezi wa mazishi

- Shughulikia masuala ya malipo ya wafanyakazi, utekelezaji wa sheria na maombi mengine ya serikali
- Jibu kesi na hatua za kisheria

## HAKI ZAKO

Ikija kwa masuala ya maelezo yako ya afya, una haki fulani. Sehemu hii inafafanua haki zako na baadhi ya wajibu wako.

*Tuulize jinsi ya kuomba yafuatayo:*

### KUPATA NAKALA YA KIELEKTRONIKI AU YA KARATASI YA REKODI YAKO YA MATIBABU

- Unaweza kuomba, kwa maandishi, kuona au kupata nakala ya kielektroniki au ya karatasi ya rekodi yako ya matibabu na maelezo yako mengine ya afya tuliyohifadhi.
- Unaweza pia kutuagiza tutume rekodi hizo kwa mshirika mwingine. Lazima utume ombi hili kwa maandishi na utueleze wazi tunapaswa kutuma nakala ya rekodi hiyo ya matibabu kwa nani na wapi.
- Tunaweza kukupa fomu inayofaa ya kusaidia kuomba nakala ya rekodi yako ya matibabu na/au kutuagiza tutume rekodi hizo kwa mshirika mwingine. Tutakupa nakala au muhtasari wa maelezo yako ya afya, kwa kawaida ndani ya siku 30 baada ya kutuma ombi lako.
- Tunaweza kukutoza ada nafuu inayofaa na hatutazuilia nakala ya rekodi zako za matibabu kwa sababu ya deni la bili ya matibabu.
- Tafadhali wasiliana na Idara ya Utoaji wa Maelezo ya Usimamizi wa Maelezo ya Afya ya kituo husika (Health Information Management Release of Information Department).

    - Utoaji wa Maelezo – 913-588-2454 au roi@kumc.edu
    - New Liberty Hospital Corporation – 816-792-7067 au recordrequest@libertyhospital.org
    - Ikiwa tovuti yako husika ya mgonjwa ina chaguo la kuomba kutolewa kwa rekodi yako ya matibabu ya kielektroniki, unaweza kutuma ombi lako kwa kufuata maagizo yaliyo kwenye tovuti ya mgonjwa.

### KUOMBA KUREKEBISHWA KWA REKODI YAKO YA MATIBABU

- Unaweza kutuomba, kwa maandishi, turekebishe maelezo yako ya afya ambayo unafikiri si sahihi au si kamili.
- Tunaweza "kukataa" ombi lako, lakini tutakupa sababu kwa maandishi ndani ya siku 60. Sababu za kukataa zinaweza kuwa ni pamoja na, lakini si tu zifuatazo:
    - Maelezo hayo hayakutengenezwa na mshiriki yeyote wa mfumo wa afya, isipokuwa iwapo mtu au mshiriki aliyetengeneza maelezo hayo hapatikani tena ili kuyarekebisha.
    - Rekodi hiyo ya matibabu si sehemu ya rekodi maalum iliyowekwa.

- Ombi hilo linahusiana na maelezo ambayo huruhusiwi kuyachunguza na/au kupata nakala yake.
- Maelezo hayo yamebainishwa kuwa ni sahihi na kamili.

## KUOMBA MAWASILIANO MBADALA

- Unaweza kutuomba, kwa maandishi, tuwasiliane nawe kwa njia maalum (kwa mfano, kwa simu ya nyumbani au ya ofisi) au tutume barua kwa anwani tofauti.
- “Tutakubali” maombi yote yanayofaa.

## KUTUOMBA TUPUNGUZE MAELEZO TUNAYOTUMIA AU KUTUMA

- Unaweza kutuomba tusitumie au tusitume maelezo fulani ya afya kwa ajili ya matibabu, malipo au kwa shughuli zetu na kwa makusudi mengine fulani. Lazima utume maombi haya kwa maandishi, lakini si lazima tukubali maombi yako (isipokuwa kama inavyoelezwa hapa chini) na tunaweza “kukataa” ikiwa yanaweza kuathiri huduma yako ya matibabu.
- Ukilipia mwenyewe gharama yote ya huduma au bidhaa ya huduma ya afya wakati wa kupokea huduma, tunatakiwa tukubali ombi lako la kutotuma maelezo hayo kwa mtoa huduma yako ya bima ikiwa kusudi la ufichuzi huo ni kwa ajili ya malipo au uendeshaji wa shughuli. “Tutakubali” isipokuwa iwe tunatakiwa tutume maelezo hayo kisheria.

## KUPATA ORODHA YA WASHIRIKI TULIOWATUMIA MAELEZO

- Unaweza kutuomba, kwa maandishi, orodha (rekodi) ya mara ambazo tumetuma maelezo yako ya afya kwa miaka sita kabla ya tarehe unayoomba, tuliyemtumia maelezo hayo na sababu ya kumtumia.
- Tutajumuisha mara zote za ufichuzi tuliofanya isipokuwa ule ambao tulifanya kwa kusudi la matibabu, malipo na/au shughuli za huduma ya afya na ufichuzi mwingine fulani (kama vile ufichuzi wowote uliotuomba tufanye). Tutakupa rekodi moja kwa mwaka bila malipo, lakini tutatoza ada nafuu inayofaa ukiomba rekodi nyingine ndani ya kipindi cha miezi 12.

## KUPATA NAKALA YA TAARIFA HII YA FARAGHA

- Taarifa hii itapatikana ukiiomba, katika ofisi zetu na kwenye tovuti yetu. Unaweza kuomba nakala ya karatasi ya Taarifa hii wakati wowote, hata kama umekubali kupokea Taarifa hiyo kielektroniki. Tutakupa nakala ya karatasi haraka iwezekanavyo.

## KUCHAGUA MTU WA KUKUWAKILISHA

- Ikiwa umempa mtu fulani uwezo wa kukuwakilisha kimatibabu au ikiwa mtu fulani ni mlezi wako rasmi, mtu huyo anaweza kutumia haki zako na kufanya maamuzi kuhusu maelezo yako ya afya.

- Tutahakikisha mtu huyo ana mamlaka haya na anaweza kukuwakilisha kabla hatujachukua hatua yoyote.

**KUWASILISHA MALALAMIKO IKIWA UNAHISI KUWA HAKI ZAKO ZIMEKIUKWA**

- Tumejitolea kulinda faragha na usiri wa maelezo yako binafsi ya afya. Ikiwa unaamini kuwa haki zako za faragha zimekiukwa, unaweza kuwasiliana nasi kwa nambari ya simu au anwani iliyowekwa mwisho wa Taarifa hii.
- Unaweza pia kuwasilisha malalamiko kwa U.S. Department of Health and Human Services Office for Civil Rights kwa kutuma barua kwa 200 Independence Avenue, S.W., Washington, D.C. 20201, kwa kupiga simu kwa nambari 877-696-6775, au kwa kutembelea HHS.gov.
- Hatutakulipiza kisasi kwa kuwasilisha malalamiko.

**CHAGUO ZAKO**

- Kwa maelezo fulani ya afya, unaweza kutuambia maelezo ambayo ungependa tuyatume.
- Ikiwa una mapendeleo ya wazi ya jinsi tunavyotuma maelezo yako katika hali zilizoelezwa hapa chini, tueleze. Tueleze unachotaka tufanye na tutafuata maagizo yako.

**KATIKA HALI HIZI, UNA HAKI NA CHAGUO LA KUTUAMBIA:**

- Tusijumuishe maelezo yako katika saraka ya hospitali
- Tutume maelezo kwa wanafamilia, marafiki wa karibu au wengine wanaohusika katika huduma yako ya matibabu
  - Tutafichua tu maelezo ya afya yanayohusiana moja kwa moja na jinsi wanavyohusika katika huduma yako ya matibabu au malipo.
  - Ikiwa huwezi kutuambua mapendeleo yako, kwa mfano, ikiwa umepoteza fahamu, tunaweza kuchukua hatua na kutuma maelezo yako ikiwa tunaamini kuwa ni kwa maslahi yako bora.

**KATIKA HALI HIZI, HATUTUMI KAMWE MAELEZO YAKO ISIPOKUWA UTUPATIE IDHINI YA MAANDISHI:**

- Makusudi ya matangazo
- Kuuza maelezo yako
- Kutuma zaidi maelezo ya tiba ya kisaikolojia

**KATIKA HALI YA KUCHANGISHA PESA:**

- Tunaweza kuwasiliana nawe kwa juhudi za kuchangisha pesa, lakini unaweza kutuambia tusiwasiliane nawe tena. Ikiwa hutaki tuwasiliane nawe kwa makusudi ya kuchangisha pesa, unaweza kuwasiliana na Timu ya Kuchangisha Pesa (Fund Development) ya The University of Kansas Health System kwa nambari 913-588-2800 au FundDevelopment@kumc.edu.

- Liberty Hospital Foundation kwa nambari 816-792-7014 au Foundation@libertyhospital.org

**TEKNOLOJIA YA MAELEZO YA AFYA YA KIELEKTRONIKI:**

- Mfumo wa afya unashiriki katika ubadilishanaji wa kieletroniki wa maelezo ya afya, ambao pia unaitwa ubadilishanaji wa maelezo ya afya (HIE, Health Information Exchange). Teknolojia hii inamruhusu mtoa huduma kutuma ombi moja kupitia shirika la maelezo ya afya (HIO, Health Information Organization) la kupata rekodi za kielektroniki za mgonjwa mahususi kutoka kwa washiriki wengine wa HIE kwa makusudi ya matibabu, malipo, shughuli za huduma ya afya na/au makusudi mengine halali. Mashirika ya HIO yanatakiwa yatumie mbinu za usalama zinazofaa ili kuzuia matumizi na ufichuzi ambao haujaidhinishwa.
- Isipokuwa ueleze vinginevyo, maelezo yako ya afya ya kielektroniki yataweza kufikiwa kupitia HIO kwa wapokeaji walioidhinishwa ipasavyo.
- Unaweza kuzuia ufikiaji wa maelezo yako kupitia HIO kwa kutuma ombi la kujiondoa kwenye HIE kupitia Teknolojia ya Maelezo ya Afya ya Kansas (KanHIT, Kansas Health Information Technology), kwa kutembelea KanHIT.org au kwa kuwasiliana na Kituo cha Usaidizi cha KanHIT kwa nambari 785-296-0461. Hata ukiamua kuzuia ufikiaji, maelezo yako bado yanaweza kutumwa kupitia HIE kwa madhumuni yanayohitajika kisheria.
    - Tafadhali elewa kuwa ukiamua kuzuia ufikiaji wa maelezo yako ya afya ya kielektroniki kupitia HIO, maelezo yako hayatapatikana kwa urahisi kupitia HIE katika hali ya dharura.
    - Zaidi ya hayo, ukiamua kujiondoa katika huduma ya kuruhusu maelezo yako kutumwa kupitia HIO haitaathiri mbinu nyingine tunazotumia kutuma maelezo yako kisheria.
    - Ukipokea huduma za afya katika jimbo lingine kando na Kansas, sheria tofauti zinaweza kutumika kuhusu uzuiaji wa ufikiaji na ubadilishanaji wa maelezo yako ya afya ya kielektroniki. Tafadhali wasiliana moja kwa moja na mtoa huduma wako wa nje ya jimbo kuhusiana na sheria hizo.
    - Kwa wagonjwa wa New Liberty Hospital pekee tafadhali piga simu kwa nambari — 816-415-3480 kwa maombi ya kujiondoa.

**UFICHUZI NA MATUMIZI YETU**

Kwa kawaida tunatumiaje au tunatumaje maelezo yako ya afya? Kwa kawaida tunatumia au kutuma maelezo yako ya afya kwa njia zifuatazo.

**KUKUTIBU**

- Tunaweza kutumia maelezo yako ya afya na kuyatuma kwa wataalamu wengine wanaokutibu.
- Tunaweza kutumia maelezo yako afya kukuambia au kupendekeza matibabu mapya mbadala au huduma nyingine zinazohusiana na afya zinazoweza kukuvutia.

*Mfano: Daktari anayekutibu jeraha anamwuliza daktari mwingine kuhusu hali ya afya yako kwa ujumla.*

## TUMA BILI ZA HUDUMA

- Tunaweza kutumia na kutuma maelezo yako ya afya ili kutuma bili na kupata malipo kutoka kwa bima za afya au washirika wengine.

*Mfano: Tunatuma maelezo yako kwa mpango wako wa bima ya afya ili mpango huo ulipie huduma ulizopokea.*

## ENDESHA SHIRIKA LETU

- Tunaweza kutumia na kutuma maelezo yako ya afya ili kuendesha shirika letu, kuboresha huduma yako ya matibabu na/au kuwasiliana nawe panapohitajika.
- Tunaweza kuwasiliana nawe kwa simu, kwa barua au kwa njia ya kielektroniki:
    - Kama kikumbusho kwamba una miadi ya huduma na matibabu
    - Kuhusu maelezo ya matibabu
    - Kukuomba ujaze utafiti mfupi kuhusu huduma na matibabu uliyopokea

*Mfano: Tunatumia maelezo yako ya afya kudhibiti matibabu na huduma unazopokea.*

## Tunaweza kutumia au kutuma maelezo yako ya afya kwa jinsi gani nyingine?

Tunaruhusiwa au tunatakiwa kutuma maelezo yako ya afya kwa njia nyingine – kwa kawaida kwa njia zinazochangia kwa faida ya umma, kama vile afya ya umma na utafiti. Lazima tutimize masharti mengi ya kisheria kabla tuweze kutuma maelezo yako kwa makusudi haya.

## FANYA UTAFITI

- Tutatumia na kutuma maelezo yako ya matibabu kwa ajili ya utafiti ikiidhinishwa kupitia utaratibu maalum ili kuhakikisha faragha ya maelezo yako ya matibabu. Tunaweza pia kutuma maelezo yako ya matibabu kwa ajili ya maandalizi ya kufanya mradi wa utafiti na kuwasiliana nawe kuhusu uwezekano wa kushiriki katika utafiti. Ikiwa hutaki tuwasiliane nawe kwa makusudi ya kushiriki katika utafiti, tafadhali piga simu kwa nambari 913-945-7397. Tutajitahidi tuwezavyo kuzuia mawasiliano haya ya kushiriki katika utafiti. Hatua ya kujiondoa haitahusika kwa matumizi ya maelezo yako ya afya kwa makusudi yaliyobainishwa katika sehemu zilizoelezwa hapo juu na haitazuia watoa huduma wako kujadiliana nawe kuhusu utafiti husika.

## TII SHERIA

- Tutatuma maelezo yako ikiwa inahitajika kulingana na sheria za jimbo au za nchi, ikiwa ni pamoja na Idara ya Afya na Huduma za Binadamu (Department of Health and Human Services) ikiwa wanataka kubaini kwamba tunatii sheria ya faragha ya nchi.

## JIBU MAOMBI YA KUCHANGA VIUNGO NA TISHU

- Tunaweza kutuma maelezo yako ya afya kwa mashirika ya kununua viungo.

## SAIDIA KATIKA MASUALA YA AFYA NA USALAMA WA UMMA

- Tunaweza kutuma maelezo yako ya afya kwa hali fulani.
    - Kuzuia au kudhibiti magonjwa, majeraha au ulemavu (kama vile sajili za magonjwa au kiwewe)
    - Kumjulisha mtu ambaye huenda ameambukizwa ugonjwa au hali fulani
    - Kuripoti data ya kuzaliwa na vifo
    - Kuwasaidia watengenezaji wa vifaa vya matibabu wanaoweza kuhitaji kuwasiliana nawe kuhusu kifaa cha matibabu kinachohitajika kwa matibabu yako na/au kurejeshwa kiwandani
    - Kuripoti athari mbaya za dawa
    - Kuripoti aina fulani za madai ya utekelezaji wa dhuluma, kutelekezwa au vurugu za nyumbani
    - Kuzuia au kupunguza hatari kubwa kwa afya na usalama wa mtu yeyote

## SHIRIKIANA NA MCHUNGUZI WA KIMATIBABU AU MWELEKEZI WA MAZISHI

- Tunaweza kutuma maelezo ya afya kwa afisa mchunguzi wa vifo, mchunguzi wa kimatibabu au mwelekezi wa mazishi mtu anapoaga dunia.

## JIBU KESI NA HATUA ZA KISHERIA

- Tunaweza kushiriki maelezo yako ya afya kutokana na agizo la mahakama au usimamizi, kibali cha upekuzi au kutokana na mwito wa kufika mahakamani.

## KUSHUGHULIKIA MASUALA YA MALIPO YA WAFANYAKAZI, UTEKELEZAJI WA SHERIA NA MAOMBI MENGINE YA SERIKALI

- Tunaweza kutumia au kutuma maelezo yako ya afya.
    - Kwa madai ya malipo ya wafanyakazi
    - Kwa makusudi ya utekelezaji wa sheria au kwa afisa wa utekelezaji wa sheria
    - Ikiwa wewe ni mfungwa wa kituo cha kurekebisha tabia au uko chini ya ulinzi wa afisa wa utekelezaji wa sheria
    - Kwa mashirika ya usimamizi wa afya kwa shughuli zilizoidhinishwa kisheria
    - Kwa shughuli maalum za serikali kama vile shughuli za kijeshi, ulinzi wa nchi na huduma za ulinzi wa rais

## WAAJIRI

- Katika hali chache, tunaweza kutuma maelezo yako ya afya kwa mwajiri wako ikiwa tunakupa huduma za afya kwa ombi la mwajiri wako na tumekupa taarifa ya huduma hizo zilizoombwa na mwajiri.

## UFICHUZI NA MATUMIZI MENGINE

- Ufichuzi na matumizi mengine ya maelezo yako ya afya ambayo hayakuelezwa katika sehemu za awali za Taarifa hii yatafanywa tu kwa ruhusa na idhini yako ya maandishi.
- Katika hali nyingine, sheria ya jimbo au nchi inaweza kututaka tupate idhini yako mapema kabla ya kufichua maelezo kuhusu hali fulani za kiafya au aina za matibabu, kama vile matatizo ya matumizi ya pombe au dawa za kulevya au afya ya akili.

## REKODI ZA UGONJWA WA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA

- Hatuwezi kutumia au kufichua maelezo yako ya afya yaliyo kwenye rekodi za matibabu ya ugonjwa wa matumizi ya dawa za kulevya tulizopokea kutoka kwa mipango ya kushughulikia ugonjwa wa matumizi ya dawa za kulevya chini ya kifungu cha 42 CFR Sehemu ya 2 (Part 2), ikijumuisha maelezo yaliyo kwenye mawasiliano tuliyopokea kutoka kwa mipango hiyo yanayotoa maelezo yaliyomo kwenye rekodi hizo, kwa kujibu ombi la rekodi zinazohusiana na kesi ya kiraia, kihalifu, kiusimamizi au kisheria inayokuhusu, isipokuwa tuwe kwanza tumepokea idhini yako ya mapema ya maandishi au amri ya mahakama ikiambatana na amri ya kufika mahakamani iliyopatikana kulingana na masharti ya Sehemu ya 2 inayotulazimisha kufichua maelezo hayo. Hatuwezi kutumia au kufichua maelezo yoyote ya afya yaliyo kwenye rekodi za ugonjwa wa matumizi ya dawa zinazopatikana katika Sehemu ya 2 kwa makusudi ya kuchangisha pesa, isipokuwa kwanza tukupe fursa wazi na dhahiri ya kuchagua kutopokea mawasiliano kama hayo yoyote ya kuchangisha pesa.

## WAJIBU WETU

- Tunatakiwa kisheria kudumisha faragha na usalama wa maelezo yako ya afya yanayolindwa.
- Tutakujulisha haraka iwezekanavyo ikiwa tukio la ukiukaji litatokea ambalo huenda limeathiri faragha au usalama wa maelezo yako.
- Lazima tufuate wajibu na mbinu za faragha zilizoelezwa katika Taarifa hii na tuwe tayari na nakala za kukupa ukiomba.

*Kwa maelezo zaidi kuhusu haki zako chini ya Sheria ya Uwajibikaji na Uwezo wa Kuhamishika kwa Bima ya Afya (HIPAA, Health Insurance Portability and Accountability Act), tafadhali tembelea* HHS.gov.

## MABADILIKO KWA MASHARTI YA TAARIFA HII

Tunaweza kubadilisha masharti ya Taarifa hii, na mabadiliko hayo yatahusu maelezo yako yote tuliyohifadhi. Taarifa mpya itapatikana ukiomba, katika ofisi zetu na kwenye tovuti yetu.

**Ili upate maelezo kuhusu jinsi ya kutuma maombi yako ya maandishi au ukiwa na maswali yoyote kuhusu Taarifa hii au mbinu zetu za faragha, tafadhali tumia maelezo ya mawasiliano yaliyowekwa hapa chini.**

**University of Kansas Hospital Authority, Afisa wa Faragha ya Mfumo**

2330 Shawnee Mission Pkwy., Suite 200
Westwood, KS 66205
913-588-2526 au upige simu isiyolipishwa kwa nambari 844-527-0597

**UKHS Great Bend, Mdhibiti wa Hatari na Afisa wa Faragha**

514 Cleveland St.
Great Bend, KS 67530
620-603-7430

**Olathe Medical Center and Miami County Medical Center, Privacy Official**

20333 W. 151st St.
Olathe, KS 66061
913-791-3548 au piga simu bila malipo kwa nambari 855-340-4200

**New Liberty Hospital Corporation, Privacy Official**

2525 Glenn Hendren Drive
Liberty, MO 64068
816-792-7231

Lugha ya Ishara ya Marekani/ASL: Ikiwa unazungumza Lugha ya Ishara ya Marekani, unaweza kupata huduma za ukalimani/tafsiri bila kulipishwa. Mfahamishe mlezi wako ikiwa unahitaji huduma za ukalimani/tafsiri. Piga simu kwa nambari 913-588-7811.

Español / Spanish: Si habla español, tiene a su disposición servicios gratuitos de asistencia lingüística. Haga saber a su médico si necesita servicios de un intérprete. Llame 913-588-7811.